Mkataba wa Utamaduni wenye Haki

Umepitishwa na muungano wa ushirikano wa kimataifa kufuatia mchakato wa ubunifu shirikishi wa kimataifa ulioratibiwa na Tume ya Ujerumani ya UNESCO

Mkataba wa
Utamaduni
wenye Haki

YALIYOMO

DIBAJI 6

MAANA YA UTAMADUNI WENYE HAKI 12

MALENGO 14

KANUNI 16

1. Masharti ya kazi yenye staha na malipo yenye haki 17

2. Ufikiaji wa uanuwai wa kitamaduni wa kujieleza na rasilimali 19

3. Kutobagua na usawa i wa kijinsia 20

4. Maendeleo ya mashinan 22

5. Ufikiaji wa Soko 23

6. Usawa wa kidijitali na maadili 25

7. Kuheshimu mazingira 26

8. Uelewa wa umma na watumiaji 27

HATUA ZA BAADAYE 28

UTAYARISHAJI WA MKATABA WA UTAMADUNI WENYE HAKI 30

VIPI NA KWA NINI KUSAINI MKATABA WA UTAMADUNI WENYE HAKI? 32

MUHURI 34

DIBAJI

Mkataba huu wa Utamaduni wenye Haki unasaidia uundaji na uimarishaji wa vuguvugu la kujenga mahusiano ya utamaduni wenye haki ndani na kati ya mataifa na kanda za ulimwengu. Mahusiano haya yanatekelezwa kwa kubainisha kanuni nane zinazolenga kukuza mazingira endelevu, ya haki na heshima kwa wasanii, wabunifu, na wafanyakazi wengine wa kitamaduni, na hivyo kulinda uanuwai wa kitamaduni duniani. Sisi, kama mashirika na watu binafsi tuliotia saini Mkataba huu, tunafanya hivyo ili kuunga mkono na kuwa sehemu ya vuguvugu hili la Utamaduni wenye Haki. Tunakaribisha mashirika mengine ya umma, ya kibinafsi na ya kiraia, vyombo vya serikali pamoja na watu binafsi kutia saini Mkataba huu. Kwa kutia saini, tunajitolea kuhuisha kanuni zake na kukuza kujulikana kwake, na kuidhinishwa kwa Mkataba.

Sisi ni sehemu ya vuguvugu hili kwa sababu tunaamini kwamba wasanii, wabunifu, na wafanyakazi wengine wa kitamaduni hutoa michango ya kipekee na yenye mageuzi kwa ustawi wa watu binafsi, maendeleo ya jamii na ustawi wa uchumi kote duniani, pamoja na kupitia ubadilishanaji wa kimataifa. Tunaamini kwamba nguvu hii ya mageuzi hutokana hasa na uwezo wa ajabu wa ubunifu wa binadamu. Katika hali zake, bidhaa na huduma za kitamaduni huwa ni za kiuchumi na kitamaduni: mbali na kuzalisha mapato na ajira, wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni hutoa mchango mkubwa kwa utambulisho, tafakuri na urithi wa tamaduni duniani kote.

Tunajitolea kutetea uhuru wa kisanii, mazingira ya kazi yenye haki, na malipo ambayo yanafaa na kutosheleza. Kwa hivyo, tunalenga kushughulikia vikwazo vyovyote vinavyowakumba wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni vinavyozuia uwezo wao wa kuwasilisha sanaa yao kwa njia huru na kujikimu kimaisha. Tunanuia kuimarisha hadhi ya kisheria ya wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni, bila kujali hali yao ya ajira au iwapo wanafanya kazi ya kandarasi; bila kujali iwapo hadhi yao ya kikazi inatambuliwa na serikali zao; na bila kujali iwapo wanafanya kazi katika miktadha ya kibiashara au isiyo ya kibiashara. Pia, tunashirikisha wajasiriamali, biashara ndogo ndogo, na za wastani, vyama vya ushirika na vikundi ambavyo utendakazi wao unawiana na Mkataba huu katika mipango yetu. Tunazingatia hasa wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni walio katika mazingira magumu na waliotengwa, tukiangazia tofauti za kimfumo na kutokuweko kwa usawa katika ushirikiano wa kitamaduni unaoendelea kuwepo katika viwango vya mashinani, kitaifa na kimataifa.

Mkataba huu unatumia msingi wa sheria za kimataifa zilizopo, hasa, Pendekezo la UNESCO la 1980 kuhusu Hali ya Msanii, Mkataba wa UNESCO wa 2005 wa Kulinda na Kukuza Uanuwai wa Kitamaduni wa Kujieleza, Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Utamaduni, sheria nyingine muhimu za kimataifa pamoja na mikataba na viwango vilivyowekwa na WIPO na ILO, na pia ajenda ya Umoja wa Mataifa ya maendeleo endelevu.

Pia inajikita kwenye taratibu zilizoko mashinani, kitaifa na kikanda ikijumuisha taratibu za kisheria na aina nyingine za utawala. Mkataba unaimarisha mifumo hiyo iliyopo kwa kujenga ubia na wadau wa ziada wasio wa kiserikali. Hilo linahakikisha ya kwamba manufaa yaliyoahidiwa ya taratibu hizi yanawafikia walengwa wanaokusudiwa, kwamba wote wanatendewa haki na kwamba kunabuniwa ahadi, ushirikiano na mahusiano madhubuti ya wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni na wadau wengine katika mifumo ya ikolojia ya sanaa na ya kitamaduni yenye usawa.

Mkataba huu unahamasishwa na mafanikio ya Mkataba wa Biashara yenye Haki na Vuguvugu la Biashara yenye Haki katika kuanzisha mahusiano ya kibiashara ya haki, kuboresha na kujipangia hali ya maisha kwa zaidi ya wakulima milioni mbili, huku ikikiri kwamba biashara ya bidhaa na huduma za kitamaduni inahitaji mbinu zinazoelekezwa mahitaji maalumu zaidi.

Mkataba huu ni suluhisho la jukumu linalozidi kuongezeka la mazingira ya kidijitali na, isitoshe, upatikanaji mwingi na ukuaji wa haraka wa mifumo ya Akili Unde wa hivi karibuni, ambayo yote mawili yameleta fursa na changamoto mpya kwa sekta za utamaduni na ubunifu. Miongoni mwa hizi ni tofauti kubwa ya kidijitali na mifumo ya biashara isiyozingatia maadili na usawa katika baadhi ya majukwaa ya kidijitali.

Mkataba huu unasisitiza umuhimu wa haki za milikidhihini katika kudumisha tija ya ubunifu, na kufanya kazi kuhakikisha wanalindwa kama inavyohitajika katika miktadha maalumu.

Kwa kuzingatia mapungufu yaliyoko katika sera za kitamaduni zilizopo katika miktadha maalumu, watia saini wote wanaunga mkono kuafikiwa kwa mahusiano ya kitamaduni yenye haki kupitia sera za kimaadili zikithamini uhuru, haki, na usawa kwa kuwa hizi zimefungamanishwa katika Mkataba huu wa Utamaduni wenye Haki.




VISA

MAANA YA UTAMADUNI WENYE HAKI

Utamaduni wenye Haki ni vuguvugu linalotaka kufikia masharti mazuri ya kazi kwa wasanii wote, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni.

Utamaduni wenye Haki unatoa wito kwa mashirika ya umma, ya kibinafsi na ya kiraia, pamoja na watumiaji na hadhira kuendeleza hali bora za mifumo ya ikolojia ya sanaa na utamaduni katika viwango vya mashinani, kitaifa, kikanda na kimataifa.

Utamaduni wenye Haki unanuia kufanya shughuli za kitamaduni na ubunifu kuwa endelevu zaidi, kuendeleza heshima kwa uanuwai wa kitamaduni na lugha, na haki za binadamu, ikijumuisha kwenye mazingira ya kidijitali, na kufanikisha mabadilishano na ushirikiano wa kitamaduni wenye usawa zaidi.

Huu ndio tunaouita Utamaduni wenye Haki.

MALENGO

Lengo la Mkataba wa Utamadini wa Haki ni kuendeleza heshima, ulinzi na utekelezi wa kijamii, kiuchumi, kitamaduni na haki nyingine za kibinadamu za wasanii, wabunifu na wafanyakazi wa kitamaduni, kwa kuhakikisha desturi za kazi zenye haki zaidi na ubadilishanaji wenye usawa zaidi katika viwango vya mashinani, kitaifa, kikanda na kimataifa, hasa kwa kufanya yafuatayo;

1. Kuendeleza na kudumisha masharti mazuri ya kazi kwa wasanii, wabunifu na wafanyakazi wa kitamaduni. Hii ni pamoja na haki yao ya kuwakilishwa katika miungano na malipo ya haki, kutambuliwa, na kufidiwa kwa kazi ya kitamaduni na ubunifu - hasa utekelezaji unaofaa wa haki za milikidhihini – pamoja na katika mazingira ya kidijitali.

2. Kuanzisha mazingira wezeshi ili kuimarisha ushindani na kutegemewa kwa muda mrefu kwa mifumo yenye thamani ya kitamaduni na kibunifu, na kwa kuzingatia uwiano wa kisera. Mazingira kama hayo yanapasa pia kuondoa ukosefu wa usawa na tofauti katika nyanja za soko na ushirikiano, na kuhakikisha ubadilishanaji wenye usawa zaidi wa huduma na bidhaa za kitamaduni duniani na upatikanaji jumuishi wa vyombo na maarifa ya kidijitali, kuimarisha kuboresha maendeleo, kuimarisha vipawa na kurasimisha sekta ikiwa ni kwa manufaa ya wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni.

3. Kushirikisha sekta ya kibinafsi, hasa mashirika ya kibiashara ya kimataifa na makampuni ya kiteknolojia, kwa ushirikiano wa kiubunifu na serikali, taasisi, za serikali, na miungano ya kiraia katika sekta mbalimbali na kanda za dunia katika utekelezaji wa kanuni za Utamaduni wenye Haki na hatua za utathmini wake.

4. Kujenga uelewa wa umma miongoni mwa watumiaji na hadhira kuhusu umuhimu wa kulinda na kuendeleza uanuwai wa kitamaduni wa kujieleza, pamoja na kulinda haki na masharti nafuu ya wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni.

KANUNI

Ili kufanikisha malengo ya Utamaduni wenye Haki, ni sharti kutambua na kutimiza majukumu yafuatayo yaliyofafanuliwa katika kanuni nane elekezi. Hii inamaanisha kujitolea kuzingatia kanuni hizi zote, na kutambua kwamba maendeleo katika nyanja fulani hayafai kuwa vikwazo kwa nyanja nyingine:

1 Masharti ya kazi yenye staha na malipo yenye haki

Utamaduni wenye Haki unahitaji heshima, ulindaji na utekelezi wa haki za binadamu za wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni. Wana haki ya kupewa heshima na hadhi yao ya kitaaluma, kijamii na kiuchumi kulindwa na kuboreshwa kulingana na sheria za kimataifa. Wana haki ya mazingira ya kazi yenye usalama, jumuishi na yenye heshima, pamoja na malipo yanayofaa na linganifu kwa matumizi ya kazi yao, yanayoandamana na ulindaji thabiti wa haki za milikidhihini. Viwango vya maadili na vya haki vya ajira kama vilivyowekwa na Shirika la Kazi Duniani vinapaswa kutekelezwa na kuzingatiwa. Viwango hivi ni pamoja na kuwekewa dhamana na kulindwa dhidi ya vihatarishi vya maisha, pamoja na matatizo maalumu kwa wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni wa jinsia ya kike kama ujauzito, uzazi, na matokeo yake. Mikataba ya pamoja kuhusu malipo inapasa kuendelezwa kama utaratibu unaofaa kutekelezwa na kutumiwa kulingana na viwango vya ajira vya sekta husika. Masharti haya yanajumuisha hasa haki za milikidhihini.

Haya ni majukumu ya pamoja na ya kibinafsi ya wadau wote wanaohusika katika sekta ya utamaduni na ubunifu; kama vile serikali, mashirika/makampuni ya umma na ya kibinafsi, makundi ya kiraia, vyama vya wafanyakazi, mashirika ya kitaaluma, mashirika ya usimamizi wa pamoja, au wataalamu binafsi. Utekelezaji wa majukumu haya unahitaji kufuatwa na utekelezaji wa sera na hatua zinazofaa zinazohusiana na kutimizwa kwa masharti mazuri ya kazi na malipo yenye haki. Sera na hatua za kutosha pia zinahitajika kwa mafunzo, hifadhi za jamii, ajira, masharti ya mapato na ushuru, kusafiri, na uhuru wa kujieleza kisanii, na pia kwa urasimishaji wa sekta ikiwa ni kwa manufaa ya wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni. Inapendekezwa kwa serikali kufikiria kutoa huduma za umma na ruzuku kutegemea utimizaji wa mazingira mazuri ya kazi na malipo yanayofaa na toshelevu.

② Ufikiaji wa uanuwai wa kitamaduni wa kujieleza na rasilimali

Kila mtu ana haki ya kuufikia uanuwai wa kitamaduni wa kujieleza na rasilimali zake. Katika mazingira ya kidijitali, ufikiaji una maana pana kuliko upatikanaji na uwezo wa kununua; unahitaji uvumbuzi wa utunzi bunifu kupitia lugha tofauti. Pia unamaanisha kuondoa ukosefu wa usawa wa kidijitali na kuhakikisha ufikiaji sawa wa rasilimali za kitamaduni zinazowezesha ushiriki katika utunzi, uzalishaji, usambazaji na ugawaji wa bidhaa bunifu.

Ufikiaji unahitaji msisitizo maalumu kwa elimu ya utamaduni na sanaa, pamoja na ufahamu wa kitamaduni tangu umri mdogo kabisa. Maarifa haya yanapaswa kujumuishwa katika viwango vyote vya elimu, yanafaa yawafikie vijana bila kujali hali yao ya kijamii au kiuchumi, na kuhimiza upatikanaji na utengaji wa maeneo ya kitamaduni na kisanii yanayolenga hasa watoto na vijana.

Haya ni majukumu ya wadau wote, pamoja na mamlaka ya umma, na mashirika ya kibiashara ya kimataifa yanayohitajika kufuata kiwango cha tathmini kilichowekwa. Inahitaji kujitolea kwa mashirika ya umma na ya kibinafsi kutambua na kushughulikia ukosefu wa usawa na vikwazo ambavyo vinaweza kuzuia ufikiaji na ushiriki.

Ufikiaji wa bidhaa mbalimbali za kidijitali unapaswa kufanywa kwa njia yenye heshima, hasa wakati ambapo bidhaa hizi zinahusu jamii zenye uwakilishi mdogo, za pembeni au zilizotengwa. Jamii za wakazi asilia zinahitaji uangalizi maalumu, na vilevile jamii za wazawa wenye usuli wa Kiafrika. Heshima kama hiyo inajumuisha kujiepusha na matumizi ya rasilimali za kitamaduni za watu wengine - kwa njia ambazo zinaweza kuwa uchukuaji wa utamaduni wa wengine - bila maridhiano awali na fidia yenye haki, huku ikitambua haja ya ubadilishanaji wa kitamaduni wenye usawa.

③ Kutobagua na usawa wa kijinsia

Hakupaswi kuwa na ubaguzi dhidi ya wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni katika hali yoyote ya ajira (pamoja na kuajiri, malipo, upandishwaji cheo, au kuachishwa kazi) au shughuli nyingine za kitaaluma.

Wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni wana heshima sawa na haki sawa bila ya kuzingatia rangi, nasaba, lugha, asili ya kitaifa, kikabila au kijamii, hali ya kiuchumi au ya kijamii ya kuzaliwa, tabaka, dini, umri, uana, jinsia, utambulisho wa kijinsia au ujibainishaji wa kijinsia, mtazamo wa kiuana, hali ya ndoa, wajibu wa mzazi, hedhi, ulemavu, hali ya afya, uanachama wa vyama vya wafanyakazi au maoni na ushirika wa kisiasa au hadhi nyingine, kwa mujibu wa sheria za haki za binadamu za kimataifa.

Uzingatiaji maalumu unapaswa kutolewa kwa mahitaji mahususi na kuwawezesha wanawake na pia wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni wanaotoka katika makundi yaliyotengwa, jamii za pembezoni, na jamii zenye uwakilishi mdogo. Watu wa jamii za kiasili wanahitaji uangalizi maalumu, na pia jamii za watu wenye usuli wa Kiafrika.

④ Maendeleo ya mashinani

Kushughulikia mahitaji ya wenyeji na maendeleo ya kitamaduni ya muda mrefu ni muhimu katika ushiriki wowote wa kitamaduni kati ya mashirika ya umma na ya kibinafsi kwa upande mmoja na wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni kwa upande mwingine. Maendeleo ya aina hiyo yanahitaji kujumlisha hali mbalimbali, ikiwa ni pamoja na lakini bila kujikita tu katika kuimarisha uwezo, uhawilisho wa ujuzi, maendeleo ya miundombinu, msaada wa vijana wabunifu na unawirishaji wa masoko endelevu mashinani.

Mashirika ya kimataifa na biashara kubwa, kwa sababu ya uwezo wao mkubwa, yana jukumu maalumu kwa ushiriki wa aina hiyo. Mashirika hayo yanapaswa kufuatilia kikamilifu mabadilishano ya ubunifu, yenye heshima na yasiyo ya kupora, na ya ushirikiano wa muda mrefu; yanapaswa kuwekeza tena sehemu ya faida zao katika mfumo wa ikolojia ya ubunifu na utamaduni wa kitaifa na wa wenyeji, pamoja na kwa manufaa ya jamii za wenyeji na kwa nia ya kuimarisha uwezo wa vyama vya ushirika na miungano ili iweze pia kuwasilisha sanaa na utamaduni wao. Katika muktadha wa Biashara yenye Haki kwa sekta nyingine maalumu, kwa mfano, ‘thamani ya juu’ inatumika kwa madhumuni hayo.

Ni muhimu kwa sekta ya umma kuanzisha sera ya kitamaduni ya umma ambayo inashinikiza maendeleo ya kitamaduni ya wenyeji na pia kuhakikisha kuwa biashara kubwa zinatimiza majukumu yaliyotajwa awali. Hili linaweza kuhitaji kuwa na michakato ya kidemokrasia na utawala jumuishi, huku ikiheshimu uhuru na uamuzi binafsi wa wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni katika maamuzi yanayohusiana na matumizi ya ‘thamani ya juu’ kwa kwa maendeleo ya sanaa na utamaduni wa wenyeji.

⑤ Ufikiaji wa Soko

Uwakilishaji wa anuwai wa utamaduni miongoni mwa wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni wote unapaswa kuwa na ufikiaji sawa wa masoko ya mashinani, kitaifa na kimataifa, pamoja na katika mazingira ya kidijitali. Uendelezaji na ubadilishanaji wa kitamaduni unapaswa kila wakati kurutubisha utunzi wa kitaifa na wa wenyeji na haupasi kamwe kutokea kama gharama inayotokana na kugunduliwa kwa utunzi bunifu huo. Katika kuwezesha ufikiaji wa soko, uangalizi maalumu unapaswa kupewa wanawake na pia wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni kutoka kwenye vikundi vilivyotengwa, jamii za pembezoni, na jamii zenye uwakilishi mdogo. Jamii za wakazi asilia zinahitaji uangalizi maalumu, na pia watu wa asili ya Kiafrika.

Upendeleo katika ujielezaji wa kitamaduni ambao hauwakilishwi sana sokoni na haswa katika ubadilishanaji wa kimataifa unabidi kuimarishwa kupitia njia zinazofaa na madhubuti, pamoja na njia nyingine mpya. Taratibu kama hizo pia zinahitajika kuwezesha na kusaidia usafiri wa wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni. Hizi ni pamoja na masharti kama vile viza zinazozingatia mahitaji mahususi, vibali vya kufanya kazi, mikataba ya haki ya ushuru, taratibu za forodha zinazoratibiwa, nyenzo za habari katika lugha za kienyeji na za kitaifa, na ufikiaji wa miundombinu ya kitamaduni na kielimu, kama vile makazi ya wasanii, matamasha ya sanaa, maonyesho ya kimataifa na programu za ubadilishanaji.

Mataifa yanafaa kujiepusha kuwa na makubaliano ya kibiashara ambayo yanaweza kuhatarisha uwezo wa kupitisha na kutekeleza sera za kitamaduni zinazolenga kulinda na kuendeleza uanuwai wa kitamaduni wa kujieleza katika taifa lao na katika mazingira ya kidijitali. Kwa mantiki hii, inapendekezwa sana kujumuishwa kwa upekee wa kitamaduni au kuuruhusu uwepo katika mikataba ya kibiashara ili kulinda maslahi haya.

VISA

⑥ Usawa wa kidijitali na maadili

Matumizi ya teknolojia za kidijitali katika tasnia za kitamaduni na kibunifu yanapaswa kila wakati kubuniwa ili kuboresha uanuwai wa kitamaduni wa kujieleza na kuimarisha ubunifu wa binadamu, na sio kuubadilisha. Hii inahusika katika hatua zote kuanzia kubuni, utayarishaji, baada ya utayarishaji hadi usambazaji wa bidhaa bunifu na ufikiaji. Inahusika haswa kutoka uundaji na utumizi wa mifumo ya Akili Unde, iwe Akili Unde zalishi au matumizi ya Akili Unde kabla au baada ya uzalishaji, uhifadhi, ugundulikaji na usambazaji wa kialgoriti.

Mikabala na sera zinazotawala matumizi ya teknolojia hizi zinapaswa kuwa za mwegemeo wa kibinadamu kwa njia ambazo zitakuwa za manufaa na za haki kwa wadau wote wanaohusika. Kama inavyoshauriwa na Pendekezo la UNESCO kuhusu Maadili ya Akili Unde, matumizi ya teknolojia hizi yanapaswa kuwiana na haki za binadamu. Yanapaswa pia kuzingatia uwazi, uwajibikaji na uelekezaji na ulindaji wa haki za milikidhihini na malipo yenye haki.

Kulinda haki, ikijumuisha haki za milikidhihini, na ulinzi wa siri, pamoja na data ya picha na alama za vidole, kunapaswa kuwa jukumu linalopewa kipaumbele na wadau wote; mikabala mipya, kulingana na maridhiano yanayofahamika, itahitajika kulenga ulindaji huu kama vile kuhakikisha umuhimu na ufanisi wayo licha ya maendeleo ya haraka ya kiteknolojia. Ufikiaji sawa wa vifaa vya kidijitali, maarifa ya kidijitali, ujuzi, na uwezo, pamoja na kutenga rasilimali ili kuziba tofauti za kidijitali, pia zinahitajika sana. Uangalizi maalumu unapaswa kuelekezwa kwenye kushughulikia vitisho vinavyotokana na ulundikaji wa nguvu ya soko katika tasnia za kiteknolojia.

⑦ Kuheshimu mazingira

Kuhakikisha uendelevu, vitendo na tabia za sekta za kitamaduni na ubunifu pia kwa haraka zinahitajika kupunguza na kushughulikia athari zao za kimazingira, pamoja na biyoanuwai na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Hili ni jukumu la pamoja la wadau wote wanaohusika, ikijumuisha serikali, mashirika/makampuni ya umma na ya kibinafsi, makundi ya kiraia, vyama vya wafanyakazi, mashirika ya kitaaluma, jumuiya za usimamizi wa pamoja, au wasanii binafsi, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni.

Hasa, athari hasi ya mazingira ya matumizi ya teknolojia za kidijitali na sherehe za kitamaduni na shughuli zilizo na athari kubwa ya kaboni inahitaji kushughulikiwa. Masuluhisho bunifu na ya kimfumo yanahitajika; kuna uwezekano kwa mikabala zaidi iliyogatuliwa. Masuluhisho yaliyosawazishwa yanapaswa kuanzishwa kama sehemu ya mabadiliko ya haki, pia yakiwa na nia ya kuhifadhi uwezo wa sekta hiyo kunawiri na kupunguza athari hasi katika maisha na haki za wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni. Kuheshimu mazingira pia kunamaanisha kutambua kuwa jamii, nchi, na kanda zina viwango sawa na uwajibikaji tofauti katika uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Kuheshimu mazingira ndani na kwa sekta za kitamaduni na ubunifu inahusisha kujenga uelewa kupitia elimu ya utamaduni na sanaa, ujielezaji wa kisanii, sherehe, na mipango inayotambua nguvu za sanaa na utamaduni katika kuibua hisia za huruma, kuhoji mafanikio yetu, kutafuta maana mpya, kufikiria mistakabali mbadala ya siku za usoni, kufanya majaribio, kuchochea na kuhimiza, na kuhamasisha hatua za kuhifadhi mazingira na mabadiliko ya jamii.

⑧ Uelewa wa umma na watumiaji

Uelewa wa umma na watumiaji hutekeleza jukumu muhimu katika kuimarisha zaidi heshima na kuthaminiwa kwa michango ya ubunifu ya wasanii, wabunifu na wafanyakazi wengine wa kitamaduni. Uelewa kama huo unaweza kuendesha juhudi zinazolenga kuwapa masharti bora ya kazi na malipo yenye haki; na kudumisha haki zao za kimsingi, ikiwa ni pamoja na katika mazingira ya kidijitali. Ni muhimu kuchukua kila fursa ya kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa kulinda tofauti katika ujielezaji wa kitamaduni, kwa kusisitiza hasa haja ya kuhakikisha ufikiaji wa viwakilishi vya kitamaduni vilivyobuniwa na kuzalishwa mashinani na kwa lugha za kienyeji.

Elimu ya utamaduni na sanaa ni zana madhubuti za kukuza ufahamu wa Utamaduni wenye Haki, hasa miongoni mwa hadhira za vijana katika mazingira ya kidijitali. Hatua zinazoelekezwa kujenga na kuendeleza utekelezaji wa vuguvugu la Utamaduni wenye Haki zinapaswa kupitishwa na kuhimizwa.

HATUA ZA BAADAYE

Mkataba huu wa Utamaduni wenye Haki unakaribisha utiaji saini na ushiriki wa wadau wote wanaoshawishika, ikijumuisha serikali, mashirika mengine ya umma, kampuni za kibinafsi, makundi ya kiraia, wasanii, wabunifu, wafanyakazi wengine wa kitamaduni, pamoja na wananchi binafsi. Kwa kutia saini Mkataba huu wa Utamaduni wenye Haki, wanaahidi na kujitolea kudumisha malengo na kanuni zake, kutekeleza au kuufasiri kisheria inavyostahili, na kuchangia kuibuka na kuimarisha vuguvugu la Utamaduni wenye Haki.

Wakati Mkataba unaelezea mfumo wote kwa kifupi, matumizi kwa sekta mahususi za kitamaduni na kibunifu, na pia katika nchi na maeneo mbalimbali, yatahitaji kupigwa msasa zaidi. Mipango au miongozo mahususi itatayarishwa, kuandikwa kupitia michakato ya wazi, shirikishi na itekelezwe kwa kushirikisha wadau wote wanaohusika katika kila muktadha maalumu.

Mkataba huu ni rasimu hai na inaruhusu marekebisho ya baadaye, haja ya kufanya hivyo ikitokea. Kila mchakato wa marekebisho utafahamishwa mapema kwa watia saini wake, kuhakikisha uwazi na ushiriki. Marekebisho yatafanywa kwa njia ya uwazi, na michakato jumuishi, kuhakikisha michakato ya maafikiano yenye ufanisi kati ya watia saini wa Mkataba.

UTAYARISHAJI WA MKATABA WA UTAMADUNI WENYE HAKI

Kundi la Wahariri la wataalamu tisa kutoka kote duniani limefafanua Mkataba wa Utamaduni wenye Haki katika zaidi ya vikao kumi vya kikazi katika mwaka wa 2023.

- Jordi Baltà Portolés, Mshauri wa Kitamaduni na Utafiti, Transit Projectes, Spain
- Brahim El Mazned, Mkurugenzi, Viza kwa Tamasha za Muziki, Morocco
- Prof. Véronique Guèvremont, Mwenyekiti wa UNESCO, Chuo Kikuu cha Laval, Canada
- Eddy Johana Gómez, Mkurugenzi wa Miradi, Llorona Records, Colombia
- Farai Mpfunya, Mkurugenzi Mtendaji, Hazina ya Utamaduni, Zimbabwe
- Eduardo Saravia, Mwanauchumi Mkuu, Sound Diplomacy, Colombia
- Anupama Sekhar, Mhifadhi, Ufadhili wa South-South Arts Fellowships 2022-2023 na Mwanachama wa Bodi, ArtsEquator, UAE/India
- Luanda Smith, Afisa Mkuu Mtendaji, NGO Creatividad y Cultura Glocal A.C., Mexi
- Katrina Stuart Santiago, Mwandishi na Mwanzilishi, PAGASA-People for Accountable Governance and Sustainable Action, Philippines

Kundi la Uhariri lilisimamiwa na Prof. Véronique Guèvremont.

Bodi ya Washauri kutoka taasisi kumi na moja ambazo zimekuwa wabia muhimu wa mwanzoni wa juhudi za Utamaduni wenye Haki wamepitisha kwa pamoja Mkataba wa Utamaduni wenye Haki kupitia maafikiano mnamo Februari 2024.

- Fairtrade International
- Fair Picture
- Goethe Institute (Germany)
- Institute for Creative Entrepreneurship & Innovation (Serbia)
- Instituto Maracá (Brazil)
- International Federation of Actors
- International Federation of Coalitions for Cultural Diversity
- International Federation of Musicians
- Kenya National Commission for UNESCO
- Korean National Commission for UNESCO
- Ministry of Culture of France
- UNESCO Chair Diversity of Cultural Expression at University Laval (Canada)

Zaidi ya wataalamu na taasisi 100 walishiriki katika hatua kadha katika mchakato huu, kupitia mashauriano ya maoni ya umma na maandishi, kutoa maoni yao kama sehemu ya Bodi ya Majaribio kuhusu Utamaduni wenye Haki na kama Wataalamu Vijana wa Utamaduni wenye Haki.

Mchakato wa kuratibu mkataba ya Utamaduni wenye Haki, kazi ya Kundi la Wahariri na lile ya Ushauri, uliratibiwa na Tume ya Ujerumani ya UNESCO.

VIPI NA KWA NINI KUSAINI MKATABA WA UTAMADUNI WENYE HAKI?

Vipi?

Rahisi sana. Kwa kuonyesha uungaji mkono wako katika tovuti ya ⌨ www.fair-culture.org.

Kwa nini?

Kwa kutia saini Mkataba, unaazimia kwamba unaunga mkono yaliyomo katika Mkataba na kwamba unaunga mkono nia yetu ya kuchukua hatua zaidi. Kutia saini kutaongeza idadi ya washirika na marafiki na hivyo uonekanaji, uaminifu na uhalali.

Kutia saini Mkataba hakujumuishi wajibu wowote wa kisheria kwako. Hata hivyo, hii ina maana pia kuwa kutia saini Mkataba si “cheti” na hakukuruhusu kutoa kauli zozote kuhusu ubora wa shughuli za biashara yako kuhusiana na Mkataba huu. Kwa kutia saini Mkataba, hukuruhusiwa kutumia nembo au lebo yake.

Nini Kingine?

Washirika ambao wamebuni Mkataba hawataki kuachia kwenye Mkataba. Wanataka kuunda mbinu ambazo wanatumaini kuwa siku moja zitaongoza kuwa na uweze-kano wa utaratibu wa uwajibikaji na hatua za kufuata, labda “cheti” na “lebo” kwa baadhi ya sekta za tasnia ya ubunifu.

MUHURI

Mhariri

German Commission for UNESCO
Martin-Luther-Allee 42
53175 Bonn, Germany

Wasiliana na

German Commission for UNESCO
T +49 (0) 228 60497 - 110
E info@fair-culture.org
www.unesco.de

Timu ya Wahariri

Dr Lutz Möller (anayehusika)
Friederike Kamm, Juliane Baumgarten,
Zsuzsanna Aszodi

Kwa ufadhili wa shirika la KNATCOM
(Kenya National Commission for UNESCO)

Mfasiri

Dkt. Kimani Njogu

Waliotathmini:
Kutoka Kenya: Dkt. Peter Githinji; Dkt. Miriam Osore; Dkt. Rayya Timmamy.

Kutoka Tanzania: Bw. Kulwa Abel Kindija (BAKITA).

Kufikia

Julai 2024

ISBN

978-3-947675-55-5

Hakimiliki

Matini za chapisho hili zina leseni ya Creative Commons License Attribution ShareAlike 4.0 International (CC BY-SA 4.0).
www.creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0/

Ruwaza

Panatom

unesco
German Commission for UNESCO

Kwa msaada wa

Federal Foreign Office

unesco
German Commission
for UNESCO